MALENGO YA MAENDELEO ENDELEVU




# Muhtasari wa Kozi

## Darasa la 1

**Chanzo:** Reimers, F. (2017). *Empowering students to improve the world in sixty lessons*. 1st ed. Createspace Independent Publishing Platform.

**Hati Miliki:** © 2017 Fernando M. Reimers. Kazi hii imeidhinishwa chini ya leseni ya kimataifa ya Creative Commons Attribution 4.0. Kutazama nakala ya leseni hii, tembeleahttps://creativecommons.org/licenses/by/4.0/ Haki zote zimehifadhiwa.

**Taarifa:** Maudhui yote yaliyomo humu yameandaliwa  na kuchapishwa kwa kujitegemea na  Programu ya Shule za Kimataifa (Global Schools Program).

SUSTAINABLE DEVELOPMENT GOALS
17 GOALS TO TRANSFORM OUR WORLD

Global Schools Program

| Muhtasari | |
|---|---|
| **Lengo kuu la kujifunza**<br>Wanafunzi wataelewa kuwa wao ni wanachama hai  wa jamii zao; Familia, tabaka, jirani , na ulimwengu. | |
| **Nguzo za Somo** | |
| **Somo la 1** | Mimi ni nani? Nini kinanifanya niwe na furaha na afya? |
| **Somo la 2** | Jamii ni nini? Kuchunguza tabaka langu, jirani yangu, nchi yangu |
| **Somo la 3** | Nini kitatokea sisi sote tusipokuwa na furaha na wenye afya? |
| **Somo la 4** | Usawa na uadilifu: sisi sote tumeunganishwa! |
| **Somo la 5** | Azimio letu juu ya  Haki za Binadamu |
| **Madhumuni ya Kujifunza** | |
| • Wanafunzi watabainisha  kuthamini na kuheshimu  utofauti wa kitamaduni.<br>• Wanafunzi watatumia mbinu  walizojifunza darasani katika jamii zao na maisha ya kila siku.<br>• Wanafunzi watafikiria namna wanavyoweza kutoa mchango wao katika jamii zao. | |

**Darasa la 1 Somo la 1**

" Mimi ni nani? Nini kinachonifurahisha na kuwa mwenye afya?"

**Muda:** Dakika 60
**Mada:** Sanaa za maonyesho, kuandika
**Viwango:** Afya Bora na ustawi (SDG 3); Elimu Bora (SDG 4)
**Imebuniwa na:** Katherine Kinnaird

**Muhtasari na Mantiki:** Somo hili linalenga kuwapa wanafunzi msingi wakujielezea na kujitambua binafsi ili wawe na nyenzo za kufikiria wengine kwenye masomo yajayo. Hii ni hatua ya kwanza katika mchakato wa wanafunzi kujiweka ulimwenguni.

**Lengo la Maelekezo:** Wanafunzi watakuwa na uwezo wa.....:

- Kujenga hali ya kujitambua na kujikubali
- Kufikiria kwa kina juu ya nini kinawafanya wao kuwa wao
- Kupata zana za kujieleza (kuandika na kusoma)
- Kuboresha uelewa juu ya ujuzi wa uandishi na mfanano wa viumbe visivyo hai kupitia sanaa

**Lengo la Uelewa:** Kujenga vyema hali asili ya wanafunzi kupenda kuelewa, wanafunzi wataelewa nini kinawafanya wawe wa kipekee, waainishe vitu wanavyovipenda na wasivyovipenda na waanze kufikiria kwa kina juu ya kwa nini wanafanya vitu kwa namna wanavyofanya?

**Maswali Muhimu:**

- Mimi ni nani?
- Nini ni muhimu kwangu? kwa nini?
- Nini ninapenda kufanya? Nini sipendi? kwa nini?
- Ninapenda kuwa nani baadae? Kwa nini?

**Madhumuni ya Wanafunzi kujifunza (Wanafunzi wataweza):**

- Kuwaambia wengine kuhusu wao
- Kujieleza wenyewe kupitia sanaa na uandishi

**Tathmini:** Mwalimu anaweza kuwauliza wanafunzi maswali muda wote wa somo ili kupima ufahamu wao. Mwalimu anaweza kufanya hivi wakati wa zoezi la ufunguzi, zoezi rasmi, na zoezi la kufunga (tazama chini). Mwalimu anaweza kutathmini kujieleza kwa wanafunzi kwa kutumia utaratibu ufuatao:

**1 - Kujielezea kwa kiasi**: Wanafunzi hueleza taarifa kidogo kuwahusu au kutoeleza kabisa
**2 - Kujielezea kwa kifupi:** Wanafunzi hueleza baadhi ya taarifa, lakini hutoa majibu ya tofauti.
**3 - Kujielezea vya kutosha**: Wanafunzi hueleza taarifa zinazowahusu wao , familia zao, marafiki zao, na mambo wanayoyapenda na wasiyoyapenda, lakini hawafafanui majibu yao.
**4 - Kujielezea vizuri:** Wanafunzi humuelezea mwalimu taarifa zinazowahusu wao, familia zao, marafiki zao, na mambo wanayoyapenda na wasiyoyapenda, lakini si kwa wanafunzi wenzao.
**5 - Kujielezea vizuri sanai:** Wanafunzi humuelezea mwalimu na wanafunzi wenzao taarifa zinazowahusu wao, familia zao, marafiki zao, na mambo wanayoyapenda na wasiyoyapenda kwa undani zaidi.

**Mpangilio wa mazoezi:**

- **Zoezi la Ufunguzi (Dakika 10)**: Mwalimu atawaandaa wanafunzi wajadiliane wenyewe kwa kusoma mtiririko wa mazoezi. Wanafunzi watainua mikono kama wanapenda zoezi. Mwalimu atachagua wanafunzi wawili walioinua mikono kuelezea kwa nini wanapenda zoezi na wanafunzi wawili ambao hawakuinua mikono kuelezea kwa nini hawakupenda zoezi.
- **Zoezi Rasmi (Dakika 30):** Wanafunzi watatengeneza mchoro wao unaoakisi wao ni nani au nini kinawafanya kuwa wao.
- **Zoezi la Kufunga (Dakika 10):** Wanafunzi wataelezea mchoro wao kwa wanadarasa ili kujenga ujuzi wao wa mawasiliano.

**Nyenzo/ vitendea kazi kwa ajili Wanafunzi:** Kulingana na darasa, muktadha na uwezo wa wanafunzi, mwalimu anaweza kuamua ama kuwaonesha wanafunzi mifano ya picha za watu wengine (k.m. picha za wasanii maarufu au picha za kibinafsi za wanafunzi wa darasa la kwanza) au kuruhusu wanafunzi kubuni picha za kibinafsi za zao wenyewe.

**Nyenzo/ vitendea kazi kwa ajili Walimu:**

- https://www.teachkidsart.net/teacher-workshop-self-portraits/
- https://www.learningforjustice.org/classroom-resources/lessons/painting-beauty-creatingselfportraits

**Daraja la 1 Somo la 2**

"Jamii ni nini: Darasa Langu, Familia Yangu, jirani yangu"

**Muda**: Dakika 60
**Mada**: Picha na Sanaa za Maonesho
**Viwango**: Kazi zenye staha na Ukuaji wa Uchumi (SDG 8); Viwanda, Ubunifu na Miundombinu (SDG 9); Kupunguza Kutokuwepo kwa Usawa (SDG 10); Miji na Jamii Endelevu (SDG 11)
**Imebuniwa na**: Tatiana Shevchenko

**Muhtasari na Mantiki:** Wanafunzi wataendelea kujiweka katika nafasi ndani ya jamii zao kwa kujichunguza wenyewe kulingana na zana ya ulimwengu unaowazunguka. Wanafunzi watatumia sanaa ya picha na maonyesho ili kuonyesha majukumu mbalimbali ya watu kwenye maisha yao.

**Lengo la Kufundishia:** Wanafunzi wataweza...

- Kujifunza kuhusu jamii wanazoishi na watu wanaojenga jamii zao
- Kuelewa muunganiko na kutegemeana kwa watu wote katika jamii
- Kukuza uelewa na heshima kwa taaluma mbalimbali ndani ya jamii zao
- Kutambua aina mbalimbali za kazi zinazofanywa nyumbani, shuleni na nje ya maeneo haya

**Lengo la Uelewa:** Wanafunzi wataelewa kwamba ulimwengu wao una watu tofauti wenye majukumu mengi tofauti na kwamba watu katika maisha yao wameunganishwa na wanategemeana na hivyo ni lazima wathaminiwe na waheshimiwe.

**Maswali Muhimu:**

- Ni watu gani waliopo kwenye maisha yangu ?
- Wana majukumu gani wanafanya?
- Je, watu katika jamii yetu wameunganishwaje?
- Je, majukumu yangu ya kila siku yanategemea/yananiunganisha vipi na jamii yangu?
- Je, nini kitatokea ikiwa watu hao wataacha kutekeleza majukumu yao ya kijamii?
- Ni kwa namna gani tunaweza tambua thamani ya watu hawa katika jamii yetu?

**Malengo ya Kujifunza ya Mwanafunzi (Wanafunzi wataweza):**

- Kufikiria kwa kina juu yao wenyewe na watu wengine katika maisha yao
- Kusimulia simulizi na kulinganisha uzoefu
- Kufanya kazi katika makundi kutunga michezo ya kuigiza
- Kuigiza mbele ya darasa
- Kulinganisha na kutofautisha uzoefu
- Kutambua majukumu mbalimbali na wajibu mbalimbali ya wanajamii wanaowazunguka

**Tathmini:** Wanafunzi watafanyiwa tathiminiwa kulingana na kiwango chao cha ushiriki katika zoezi.

**3 - Ushiriki kikamilifu:** Mwanafunzi anawasiliana vizuri, anafanya kazi vizuri na wengine, anachangia mjadala wa somo na kikundi chake, anashiriki katika utayarishaji wa mchezo na uchezaji.
**2 — Ushiriki wa wastani:** Mwanafunzi anasikiliza kwa makini lakini hachangii, anafanya kazi na wengine, anashiriki katika majadiliano ya darasa, ana nafasi katika igizo lakini hachangii uundaji wa igizo.
**1 - Ushiriki hafifu:** Mwanafunzi hawezi sikia au kuchangia na wenzake, mwanafunzi hawezi kuwasiliana na timu yake, mwanafunzi hawezi kufanya maonesho au kushiriki katika utayarishaji wa igizo.

**Mpangilio wa Mazoezi:**

**Sehemu ya 1: Kuchangia na Kuchora Ramani (Dakika 10)**

Mwalimu na mwanafunzi hukaa kwenye duara la majadiliano.
Mwalimu huwauliza wanafunzi: "Ni shughuli gani mnafanya kila siku?"
Wanafunzi watachangia majibu yao: kwa mfano. "Ninakunywa chai, , ninapanda basi, ninavaa nguo , ninaenda shule, nk."

Mwalimu anawauliza wanafunzi kufafanua majibu yao mfano. “Nani anakusaidia kwenye majukumu haya? Je, vitu unavyotumia kwa shughuli zako za kila siku vinatoka wapi? Unawasiliana na nani kila siku?"
Wanafunzi hujibu: mfano. "Mama yangu huniandalia kifungua kinywa asubuhi, mwalimu wangu hunifundisha, sare zangu za shule hutengenezwa na nyanya yangu / huwa nanunua sare za shule dukani, dereva wa basi hunipeleka shuleni, nk."

**Sehemu ya 2**: **Maigizo (Dakika 40)**

**2.1 - Kazi ya kundi (Dakika 10)**

- Wanafunzi wanagawanywa katika makundi madogo ya watu 2-3.
- Kila aliye kwenye kundi atawasilisha tukio kutokana na ratiba yake ya kila siku na nini ingekuwa bila uwepo wanajamii wamuhimu wanaohusika katika ratiba hii.
- Wanakikundi wataigiza namna ratiba zao zingekuwa bila uwepo wa watu muhimu katika maisha yao, au vitu muhimu au shughuli ambazo hufanywa na watu mbalimbali kwenye jamii.
- Kila kikundi kitachagua tukio moja la kuigiza.

Mfano wa igizo:
**Mazingira:** Mji Mdogo, Asubuhi

**Mwanafunzi 1 (Mwanafunzi)**: Niko tayari kwenda shule. Ninaelekea kwenye kituo cha basi na ni siku nzuri. Ninapanda basi kwenda shuleni kila asubuhi; ni njema!

**Mwanafunzi 2 (Dereva wa Basi):** Ninaendesha basi kila asubuhi, lakini leo ninaumwa. Sitaweza kuwapeleka watoto wote shuleni.

**Mwanafunzi 1 (Mwanafunzi):** Ninasubiri basi, lakini halijafika. Sidhani kama nitaweza kwenda shuleni leo.

**Mwanafunzi 3 (Mwalimu):** Nina wasiwasi sana kuhusu wanafunzi wangu. Natumaini wako sawa. Hakuna aliyekuja darasani leo.

**Mwanafunzi 1 (Mwanafunzi):** Leo lilikuwa darasa pendwa kwangu. Tulikuwa tujifunze juu ya Kasa, lakini sitaweza kufanya hivyo. Natumaini dereva wa basi yuko sawa!

**Mwanafunzi 2 (Dereva wa Basi):** Ninapenda kuwapeleka watoto wa mtaani kwetu shuleni. Natamani kwenda kazini kesho ili waende kwenye masomo yao na kujifunza mambo mengi mazuri.

**2.2 Mawasilisho ya Igizo (Dakika 30)**

- Makundi ya wanafunzi 3 (jumla ya makundi 10 kulingana na idadi ya wanafunzi 30 wa darasa) huigiza michezo yao.

**Sehemu ya 3: Majadiliano (Dakika 10)**

Baada ya kila kikundi kufanya maigizo yao mwalimu atawauliza wanafunzi maswali ya uelewa juu ya majadiliano. Kisha mwalimu ataeleza juu ya kuwazungumzia watu kwenye jamii zetu wanaotusaidia.

- Je tunafanya vitu vya aina gani kila siku?
- Ni nani walikuwa wanajamii wa muhimu kwenye maigizo tuliyoyaona?
- Ni aina ipi ya kazi, vifaa na sare wanajamii hawa wanatumia? Je, tuna uhusiano wa aina gani kati yetu na wanajamii tofauti tofauti?
- Je, nini kingetokea kama baadhi ya wanajamii wasingekuwa sehemu ya jamii ?
- Je, ni mfanano upi na tofauti zipi tunazoziona katika jamii zetu na katika ratiba zetu za kila siku?
- Je, tunawathamini vipi wanajamii wetu kila siku?

**Nyenzo kwaajili ya Wanafunzi*:**
- https://www.youtube.com/watch?v=VrBrpSTwPK8
- https://www.youtube.com/watch?v=7hEYtozmb5o
- https://www.youtube.com/watch?v=r2myzbWQIJA

*Nyenzo za wanafunzi zinategemea muktadha na uunganishwaji wa mtandao na uelewa wa lugha ya Kiingereza.

**Nyenzo kwaajili ya Waalimu::**
- Maeneo na jamii ulimwenguni: https://www.dpi.nc.gov/media/7187/open
- Jamii mahali watu wanapoishi: http://tiny.cc/G1L2R4
- Mawazo ya somo: Wasaidizi wa jamii: http://tiny.cc/G1L2R5
- Mawazo bunifu ya wasaidizi wa jamii: http://tiny.cc/G1L2R6
- https://www.lessonplanet.com/teachers/communities-around-the-world
- https://www.education.com/lesson-plan/houses-and-homes/
- https://education.nationalgeographic.org/resource/africa-physical-geography/

**Darasa la 1 Somo la 3**
"Ukosefu wa usawa"

**Muda wa muda:** dakika 60
**Mada:** Hisabati, Sayansi
**Viwango:** Kukomesha Njaa (SDG 2); Kufikia Usawa wa Kijinsia na Kuwawezesha Wanawake na Wasichana Wote (SDG 5); Kupunguza Ukosefu wa Usawa Ndani na Miongoni mwa Nchi (SDG 10)
**Imebuniwa na:** Kara Howard

**Muhtasari na Mantiki:** Somo hili linawapa nafasi wanafunzi kujihusisha kikamilifu na suala la ukosefu wa usawa na litaweka suala hili ndani ya mfumo mkubwa wa kujenga watu wenye maadili, huruma na uadilifu.

**Lengo la Kufundishia:** Wanafunzi wataweza...
- Kutambua na kuthamini kutegemeana kwa watu wote
- kujifunza namna ya kuwa mtu mwema
- Kutambua uwepo wa uhaba wa maji, nishati, na chakula
- Kupata uelewa wa kazi na majukumu katika mazingira ya kuuunganika
- Kuunganisha tunu za maadili kwenye mada ya maarifa.

**Lengo la Uelewa:** Wanafunzi wataelewa ukosefu wa usawa ni nini na nini kitatokea kama mtu ataathirika na ukosefu wa usawa. Wanafunzi wataanza kuuliza kwanini ukosefu wa usawa kunatokea na kama itadhibitishwa..

**Maswali Muhimu:**
- Ukosefu wa usawa ni nini?
- Je, ukosefu wa usawa unatufanya tujihisi vipi?
- Tunaionaje hali ya ukosefu wa usawa katika jamii zetu?
- Kwa nini ukosefu wa usawa hutokea?

**Malengo ya Kujifunza ya Mwanafunzi (Wanafunzi wataweza):**
Kutambua mifano ya ukosefu wa usawa
Kujadili hisia zinazohusiana na ukosefu wa usawa
Kukisia kwanini ukosefu wa usawa hutokea

**Tathmini:** Walimu wanaweza kutumia vipimo visivyo rasmi kwa ajili ya uelewa wakati wa zoezi, kisha kurasmisha tathmini katika mjumuisho wa mwisho wa hisia ambazo wanafunzi wanazihusisha na ukosefu wa usawa.

**Mpangilio wa Mazoezi:**

**Utangulizi:** Mwalimu atatambulisha mada ya ukosefu wa usawa kama dhana ya baadhi ya watu kuwa na kitu, pindi wengine hawana. Mwalimu atahusisha ukosefu wa usawa na dhana ya Hisabati ya uwiano usio sawa kwa kutumia alama ya $<$ kwa kutumia mifano ya $4 < 6$, $2 < 4$, n.k. Kisha Mwalimu atatumia mifano hii kuzungumzia juu ya kiasi cha vitu visivyo sawa vinaweza kuonekana katika maisha yetu ya kila siku.

**Maoezi:** Mwalimu atawambia wanafunzi kwamba wameleta peremende/pipi darasani. (Mwalimu anaweza kuleta aina yoyote ya peremende/pipi au vitafunwa vinavyotumika kwa muktadha na vinaweza kugawanywa katika vipande vidogo,( k.m. Big G, M&Ms, tofi, pretzels, n.k.) Mwalimu atawaeleza wanafunzi kwamba darasa litaona namna tunavyoweza kuwa na nyakati za ukosefu wa usawa maishani mwetu na tutafanya zoezi ambalo litatupa nafasi ya kuzungumzia jinsi tunavyohisi ukosefu wa usawa unapotokea.

* Hakikisha unawaambia wanafunzi hawapaswi kula vitafunwa hadi mwisho wa zoezi.

**Mwalimu ata:**

- Gawa vitafunwa vingi kwa mtu mmoja, na kitafunwa kimoja kwa kila mtoto darasani.
- Wawezeshe watoto waelezee ugawajii huu wa vitafunwa - pindi ukiwa sawa au si sawa.
- Waulize wanafunzi wachache walio na kitafunwa wazungumzie jinsi wanavyojisikia wanapopata kitafunwa ukilinganisha na wanafunzi wanaopata vingi.
- Muuliza mwanafunzi aliye na vitafunwa vingi kuzungumzia jinsi anavyojisikia katika hali hiyo.
- Kusanya vitafunwa vyote na kisha vigawe tena. Muda huu mwalimu atagawanya idadi sawa ya vitafunwa kwa kila wavulana darasani, lakini wasichana hawakupata vitafunwa.
- Pata majibu kutoka kwa wanafunzi wa pande zote mbili wakijadili hisia zao juu ya ugawaji huu wa vitafunwa. Mwalimu atauliza maswali kama: Je, ni sawa kwa wavulana kupata vitafunwa zaidi kuliko wasichana? Kwa nini si sawa?
- Kusanya vitafunwa vyote kwa mara ya mwisho. Urudiaji wa ugawaji wa vitafunwa utakuwa na wanafunzi 2 wenye vitafunwa vingi, wanafunzi wengine wachache (kati ya 5-10 kulingana na ukubwa wa darasa) na vitafunwa 4-5, na kisha wanafunzi wengine (wengi) kwa kitafunwa 1 tu.
- Mwalimu atawauliza tena wanafunzi kwa mara ya pili mitazamo yao juu ya ugawaji wa vitafunwa. Mwalimu atahimiza maswali kama vile "Je, hii ni haki?"

**Hitimisho:** Mwalimu ataongoza mjadala kwa kuwaomba wanafunzi kujifanya kama walichokuwanacho si vitafunwa, bali maji, au chakula. Mwalimu atawahimiza wanafunzi kufikiria itaonekanaje ikiwa wanafunzi walio na vitafunwa vingi wangekula milo 3 kwa siku, wakati watu wenye kitafunwa kimoja walikula mlo 1. Wanafunzi watajadili jinsi ambavyo wangehisi katika hali hiyo. Wanafunzi watajadili mambo mengine wanayoona ulimwenguni ambayo hayajagawanywa kwa usawa - maji, chakula, pesa, vifaa vya kuchezea, nguo, n.k. Hatimaye wanafunzi watajadili ni ugawaji gani utawanufaisha watu wote.

**Nyenzo kwaajili ya Waalimu:**

- https://www.youtube.com/watch?v=6DlQq2xLw_0
- https://www.youtube.com/watch?v=-5wo1ArN88w

**Darasa la 1 Somo la 4**

"Usawa na Haki"

**Muda:** Dakika 50

**Mada:** Elimu ya Uraia, Maarifa ya Jamii

**Viwango:** Kukomesha Umaskini (SDG 1); Kukomesha Njaa (SDG 2); Kazi Bora na Ukuaji wa Uchumi (SDG 8); Kupunguza Kutokuwepo kwa Usawa (SDG 10); Amani, Haki, na Taasisi Thabiti (SDG 16)

**Imebuniwa na:** Nicolás Buchbinder

**Muhtasari na Mantiki:** Somo hili linawasaidia wanafunzi kuanza tafakari juu ya usawa na haki. Kwa kuzingatia Somo la 3, wanafunzi watawezeshwa kufikiria kuhusu rasilimali za usawa ikiwa kama kuna muktadha mahususi ambayo yatahitaji ugawaji wa aina tofauti.

**Lengo la Kufundishia:** Wanafunzi wataweza...

- Kuelewa haki ya kila binadamu zinazopelekea maisha yenye furaha, afya na tija bila kujali jinsia, umri, ulemavu, n.k. (mfano bila umaskini, bila njaa, n.k.)
- Kuelewa itikadi ya msingi wa usawa kwa watu wote na uwezo wao

**Lengo la Kuelewa:** Wanafunzi watajenga uelewa wao juu ya usawa na haki, kupitia na kutambua nyakati na hali ambazo kila mtu anapaswa kupata matunzo ya kipekee.

**Maswali Muhimu:**

- Kukosekana kwa usawa huleta hisia gani?
- Ni vitu gani ambayo kila mtoto anapaswa kuwa nayo?
- Je, tunapaswa kutendewa sawa kila wakati?

**Malengo ya Kujifunza kwa Mwanafunzi (Wanafunzi wataweza):**

- kupendekeza na kutambua aina za vitu ambavyo kila mtoto anapaswa kuwa navyo
- Kutafsiri tatizo lililowasilishwa katika kipande cha fasihi ya watoto au video
- Kuelewa kuwa kutendewa sawa kunaweza kutegemea mazingira

**Tathmini:** Mwalimu anapaswa kuhimiza ushiriki wa wanafunzi wote ili kuhakikisha kuwa kila mmoja anahusika katika kufikiria mada.

**Mpangilio wa Mazoezi:**

**Ufunguzi (dakika 5): Kukumbuka kilichotokea katika darasa lililopita**

Mwalimu atawauliza wanafunzi wakumbuke walichofanya darasa lililopita: Ni nini kilifanyika na vitafunwa na jinsi zoezi hilo iliwafanya wajisikie katika nyakati tofauti darasani?

**Zoezi #1 (dakika 15): Kutafakari juu ya usawa**

Mwalimu atawauliza wanafunzi ni ipi njia bora ya kugawa vitafunwa, akiwaongoza wanafunzi kutafakari juu ya ugawaji uliosawa. Baada ya hapo, mwalimu atawauliza wanafunzi ni vitu gani wanafikiri kila mtoto anapaswa kuwa navyo, na ikiwa kama kila mtoto akiweza kuvipata vitu hivyo.

**Zoezi #2 (dakika 20): Haki siku si siku zote hupewa sawa kwa kila mtu**

- Mwalimu atasoma “The Fairest Teacher of Them All”
    - https://www.thephilosophyman.com/wp-content/uploads/2018/01/Philosophy_for_Readers_-_Fairest_Teacher.pdf
- Mwalimu atawauliza wanafunzi maswali tofauti kuhusu simulizi: Ni nini kilitokea katika simulizi? Kwa nini Albert alibadilisha kazi yake? Je, Albert alifanya sawa kumtendea kila mtu sawa?Nini Albert alipaswa kufanya?

**Zoezi #3 (dakika 10): Kushirikishana**

- Katika dakika 10 za mwisho, baadhi ya wanafunzi watashirikisha walichofanya na mwalimu atafunga kwa ufafanuzi na tafakari juu ya usawa na haki.

**Nyenzo kwaajili ya Waalimu:**

- https://www.thephilosophyman.com/wp-content/uploads/2018/01/Philosophy_for_Readers_-_Fairest_Teacher.pdf

**Darasa la 1 Somo la 5**

"Tamko Letu la kipekee juu ya Haki za Binadamu"

**Muda:** Dakika 60+
**Mada:** ELA, Maarifa ya Jamii
**Viwango:** Kupunguza Kutokuwepo kwa Usawa (SDG 10); Amani, Ustawi , na Taasisi Imara (SDG 16)
**Imebuniwa na:** Chloe Suberville

**Muhtasari na Mantiki:** Somo hili linawapa nafasi wanafunzi kuchukua hatua juu ya ujuzi waliopata, na kutumia maarifa yao ya usawa na ukosefu wa usawa. Kama jamii watafanya kazi kwa pamoja na kwa kuwasiliana kutengeneza tamko la haki za binadamu kama sehemu ya jamii yao ya darasani.

**Lengo la Kufundishia:** Wanafunzi wataweza kufanya kazi kwa pamoja ili kutumia maarifa yao ya usawa na ukosefu wa usawa, na nini humaanisha kuwa sehemu pana ya jamii.

**Lengo la kuelewa:** Wanafunzi wataelewa maana ya kuandaa waraka ambapo sote tunakubaliana juu ya mambo ambayo wanadamu wanastahili. Wanafunzi watafanya kazi pamoja kuandaa waraka unaoendana , kwa manufaa mapana ya jamii (darasa) ambapo wataelewa umuhimu wa waraka kama huo.

**Maswali Muhimu:**

- Tamko la haki za binadamu ni nini?
- Kwa nini ni muhimu kufanya kazi kwa pamoja?
- Tunawezaje kufanya kazi kwa pamoja?
- Ni kwa namna gani tunaweza kukubaliana nini kiandikwe kwenye waraka huu?
- Ni kwa namna gani tuwasilishe i haki zote za binadamu tunazokubaliana?

**Malengo ya Kujifunza ya Mwanafunzi (Wanafunzi wataweza):**

- Kufanya kazi kwa makundi ili kufikia lengo moja
- Kupata zana za kujielezea
- Kutumia maarifa yao juu ya usawa na haki
- Kulinganisha tunu za kimaadili zilizomo katika maarifa

**Tathmini:** Mwalimu atakuwa akizunguka wakati wa kuandaa tamko la darasa juu ya haki za binadamu, akihakikisha wanafunzi wanafanya kazi kwa pamoja. Tathmini ya mwisho itakuwa tamko kuu la haki za binadamu.

**Mpangilio wa Mazoezi:**

**Ufunguzi (dakika 10):**

- Mwalimu atawauliza wanafunzi wanakumbuka nini kuhusu kuwa sehemu ya jamii.
- Nini humaanisha  kuwa sawa? Kutokuwa sawa?
- Ni njia zipi zitatufanya  sisi sote tuwe wanajamii wenye furaha?
- Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu (UDHR) (dakika 10) Mwalimu atawasilisha baadhi ya vifungu vya UDHR (toleo lililorahisishwa) kwa wanafunzi na kujadili jinsi vilivyoandaliwa , akieleza kuwa watu wengi walikusanyika pamoja  kuandaa waraka ambao utasaidia watu wote kutendewa vyema, na ambapo watakuwa na furaha kwenye sayari..

**Demokrasia (dakika 5):**

- Mwalimu ataeleza kuwa  watakuja na mambo yatakayo kuwa ya kweli kwenye darasa lao , kwa kuzingatia  walichojifunza katika masomo yaliyopita, na watatengeneza waraka kwa pamoja.
- Mwalimu ataeleza kuwa wanafunzi watapiga kura, hivyo watakapokubaliiana na jambo wanapaswa wanyooshe mikono na kama wengi wataunga mkono jambo hilo linaweza kujumuishwa katika waraka.

**Kuandaa  vifungu (dakika 10):**

- Wanafunzi wataandaa  vifungu 10 vya tamko lao la haki za binadamu. Ikiwa wanafunzi wengi watakubaliana na kifungu  wanaweza kukijumuisha katika waraka.
- Wanafunzi wanapaswa kuhamasishwa kufikiria juu ya namna ya kawaida ya kuandaa vifungu vya haki wanvyokuja navyo, na  kuhakikisha  mawazo ya wanafunzi wote yanajumuishwa.

**Tamko lililokamilika la Kimataifa la Haki za Binadamu (UDHR ) (dakika 10):**

- Wanafunzi watawekwa katika makundi ya  watu 2-3, na watatoa, na kuandika maneno kwa kila vifungu walivyoandaa. Kila kundi litajikita kufanyia kazi kifungu kimoja cha waraka, na kitawasilisha mawazo yao kwa kutumia maneno na picha.
- Kisha mwalimu ataunganisha pamoja picha zote na kutengeneza waraka mmoja wa tamko la darasa la haki za binadamu.
- Mwalimu atamaliza somo na kutoa hitimisho.

**Nyenzo kwaajili ya Waalimu:**

- Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu (Toleo lililorahisishwa): https://www.ohchr.org/en/universal-declaration-of-human-rights